

GAZETI LA SERIKALI NA. 154 la tarehe 25/3/2022

SHERIA YA MAJISAFI NA USAFI WA MAZINGIRA
(SURA YA 272)

AMRI

(Imetolewa chini ya kifungu cha 28(d))

AMRI YA MAMLAKA YA MAJISAFI NA USAFI WA MAZINGIRA TABORA ("TABORA WSSA"), YA KUREKEBISHA BEI YA HUDUMA ZA MAJISAFI NA USAFI WA MAZINGIRA, LA MWAKA 2022

- Jina
1. Amri hii litajulikana kama, Amri ya Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Tabora ("Tabora WSSA"), (ya Kurekebisha Bei ya Huduma za Majisafi na Usafi wa Mazingira), ya Mwaka 2022.
- Bei na ada
2. Bei ya majisafi na usafi wa mazingira za "Tabora WSSA" zinarekebisha kulingana na Jedwali la Kwanza la Amri hii.
- Masharti
3. Bei zinazotolewa zinaidhinishwa pamoja na masharti yafuatayo:
- (a) kabla ya kuanza kutekeleza Bei zilizoidhinishwa, ada na malipo, Tabora WSSA iwasilishe EWURA vielelezo kwamba ilitoa taarifa kwa wateja wake kuhusu bei mpya za huduma zake na pia ilitoa elimu kikamilifu kwa umma ikiwa ni pamoja na wawakilishi wa wananchi, serikali na viongozi wa dini katika eneo lake la huduma;
 - (b) ifikapo au kabla tarehe 31 Machi 2021, "Tabora WSSA" itawasilisha EWURA Mpango wa Biashara ambao umejumuisha bei zilizoidhinishwa na mpango wa utekelezaji wa masharti ya Amri hii;
 - (c) Tabora WSSA, kwa kutumia mapato yatokanayo na bei zilizoidhinishwa, itatekeleza miradi iliyoainishwa katika Jedwali la Pili la Amri hii;
 - (d) Tabora WSSA itafikia viashiria vya utendaji kama ilivyooneshwa kwenye Jedwali la Tatu la Amri hii;
 - (e) ifikapo au kabla ya tarehe 31 Machi 2021, Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Tabora itawasilisha EWURA Mpango wa Ufuatiliaji wa Ubora wa Maji ulioandaliwa kwa kuzingatia Mwongozo wa Ufuatiliaji wa Ubora wa Majisafi na Majitaka kwa Mamlaka za Majisafi na Usafi wa Mazingira;
 - (f) Tabora WSSA itawajulisha wateja wake kuhusu mabadiliko ya bei angalau miezi mitatu kabla ya kufanya mabadiliko na kupeleka ushahidi EWURA;

Amri ya Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Tabora (“Tabora Wssa”), ya Kurekebisha Bei ya Huduma za Majisafi na Usafi wa Mazingira
Tangazo La Serikali Na. 154 (Linaendelea)

- (g) Tabora WSSA, kwa kila mwaka kama sehemu ya taarifa yake ya utendaji ya mwaka, itawasilisha EWURA taarifa ya utekelezaji wa masharti yaliyopo kwenye Amri ya bei na kila kifungu cha gharama katika mahitaji ya fedha kama ilivyoainishwa katika Jedwali la NNe; na
- (h) Tabora WSSA itaendelea kuwasilisha EWURA taarifa zake za fedha na utendaji kwa mujibu wa matakwa ya EWURA. Taarifa hizi zitatumika na EWURA katika kufanya tathmini ya utendaji wa Tabora WSSA ikilinganishwa na Mamlaka nyingine za Majisafi na Usafi wa Mazingira na uboreshaji wa huduma zake. Pia tathmini hii itazingatiwa na EWURA katika kufanya tathmini ya vigezo vya maombi yajayo yatakayowasilishwa na Tabora WSSA katika siku zijazo.

Kufuta Amri
TS Na. 41 la 2018

5. Amri hii inafuta Amri ya bei za Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Tabora iliyotangazwa kupitia Gazeti la Serikali Na. 41 la tarehe 9 Februari, 2018.

JEDWALI LA KWANZA

(Limetengenezwa chini ya aya ya 2)

BEI, ADA NA TOZO ZILIZOIDHINISHWA

Jedwali Namba 1(a): Bei za Maji za Sasa na Zilizoidhinishwa kwa Wateja Wenye Dira

Kundi la Wateja	Matumizi (m ³)	Kizio	Bei ya Sasa	Bei Zilizoidhinishwa		
			2019/20	2020/21	2021/22	2022/23
Majumbani	Wote	Shilingi kwa Ndoo ya Lita 20	24	30	35	39
	0-10	Sh./m ³	1020	1,520	1,770	1,950
	11-15		1200			
	>15		1355			
Nyumba za Ibada	Wote	Shilingi kwa Ndoo ya Lita 20	24	30	35	39
		Sh./m ³	1200	1,520	1,770	1,950
Taasisi	Wote	Shilingi kwa Ndoo ya Lita 20	26	32	43	55
	0-15	Sh./m ³	1200	1,610	2,150	2,780
	>15		1275			
Biashara	Wote	Shilingi kwa Ndoo ya Lita 20	44	52	57	57
	0-15	Sh./m ³	1685	2,640	2,860	2,870
	>15		2180			

Amri ya Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Tabora ("Tabora Wssa"), ya Kurekebisha Bei ya Huduma za Majisafi na Usafi wa Mazingira
Tangazo La Serikali Na. 154 (Linaendelea)

Viwanda	Wote	Shilingi kwa Ndoo ya Lita 20	46	56	57	58
	0-15	Sh./m ³	2180	2,820	2,860	2,900
	>15		2295			
Magati	Wote	Shilingi kwa Ndoo ya Lita 20	20	30	30	30
Wastani wa Bei		Sh./m ³	1,318	1,621	1,945	2,246

Jedwali Namba 1(b): Bei za Majitaka za Sasa na Zilizoidhinishwa (Shilingi/ Mita ya Ujazo)

Kundi la Wateja	Bei ya Sasa	Bei Zilizoidhinishwa		
	2019/20	2020/21	2021/22	2022/23
Majumbani	400	600	750	750
Taasisi	825	925	1050	1050
Biashara	825	925	1050	1050
Viwanda	1000	1250	1375	1375

Jedwali Namba 1(c): Bei za Majitaka za Sasa na Zilizoidhinishwa kwa Wateja Wasio na Maunganisho ya Majisafi (Shilingi/ Mwezi)

Kundi la Wateja	Bei ya Sasa	Bei Zilizoidhinishwa		
	2019/20	2020/21	2021/22	2022/23
Majumbani	6,000	6,000	6,000	6,000
Taasisi	28,000	28,000	28,000	28,000
Biashara	28,000	28,000	28,000	28,000
Viwanda	28,000	28,000	28,000	28,000

Jedwali Namba 1(d): Ada za Sasa na Zilizoidhinishwa za Maunganisho Mapya ya Majisafi (Shilingi/ Maunganisho)

Kundi la Wateja	Ada ya Sasa	Ada Iliyoidhinishwa		
	2019/20	2020/21	2021/22	2022/23
Majumbani	30,000	Asilimia 20 ya Gharama za Maunganisho kama Iliyoelekezwa katika Kifungu cha 26 cha Kanuni za Maji za Mwaka 2019		
Taasisi	40,000			
Biashara	40,000			
Viwanda	60,000			

Jedwali Namba 1(e): Ada za Sasa na Zilizoidhinishwa za Kurejeshwa Huduma ya Majisafi Baada ya Kukatiwa (Shilingi/ Marejesho)

Kundi la Wateja	Ada ya Sasa	Ada Zilizoidhinishwa		
	2019/20	2020/21	2021/22	2022/23
Majumbani	25,000	15,000	15,000	15,000
Taasisi	40,000	15,000	15,000	15,000
Biashara	40,000	15,000	15,000	15,000
Viwanda	60,000	15,000	15,000	15,000

Amri ya Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Tabora (“Tabora Wssa”), ya Kurekebisha Bei ya Huduma za Majisafi na Usafi wa Mazingira
Tangazo La Serikali Na. 154 (Linaendelea)

Jedwali Namba 1(f): Ada za Sasa na Zilizoidhinshwa za Maunganisho Mapya ya Majitaka (Shilingi/ Maunganisho)

Kundi la Wateja	Ada yaSasa	Ada Iliyoidhinshwa		
	2019/20	2020/21	2021/22	2022/23
Majumbani	30,000	Asilimia 20 ya Gharama za Maunganisho kama Iliyoelekezwa katika Kifungu cha 26 cha Kanuni za Maji za Mwaka 2019		
Taasisi	40,000			
Biashara	40,000			
Viwanda	60,000			

Jedwali Namba 1(g): Ada za Sasa na Zilizoidhinshwa za Kurejeshwa Huduma ya Majitaka Baada ya Kukatiwa (Shilingi/ Marejesho)

Kundi la Wateja	Ada ya Sasa	Ada Zilizoidhinshwa		
	2019/20	2020/21	2021/22	2022/23
Majumbani	20,000	25,000	25,000	25,000
Taasisi	40,000	40,000	40,000	40,000
Biashara	40,000	40,000	40,000	40,000
Viwanda	60,000	60,000	60,000	60,000

Jedwali Namba 1(h): Ada za Sasa na Zilizoidhinshwa za Kumwaga Majitaka Katika Mabwawa ya Tabora WSSA (Shilingi/ Mita ya Ujazo)

Kundi la Wateja	Tozo ya Sasa	Tozo Zilizoidhinshwa		
	2019/20	2020/21	2021/22	2022/23
Magazi ya Majitaka	1,500	1,650	1,775	1,775

JEDWALI LA PILI

(Limetengenezwa chini ya aya ya 3(c))

MIRADI ITAKAYOTOKELEZWA

Maelezo ya Kazi zitakazofanyika	TZS		
	2020/21	2021/22	2022/23
Ukarabati na Ununuzi wa Vifaa			
Kukarabati kilometa 4.8 za bomba kuu la Kazima lenye upana wa milimita 300		109,385,316	220,318,457
Kununua pampu mpya na kubadili pampu mbili Igombe zenye uwezo wa 450 m ³ /h kwenye kimo cha mita 30 na 700m ³ /h	50,000,000	89,182,849	226,533,550

Amri ya Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Tabora (“Tabora Wssa”), ya Kurekebisha Bei ya Huduma za Majisafi na Usafi wa Mazingira
Tangazo La Serikali Na. 154 (Linaendelea)

Kuboresha vifaa vya maabara na ili kuongeza uwezo wa kutibu maji na kupima ubora	-	19,533,092	39,342,582
Kununua magari manne (4)	-	222,890,552	448,935,051
Kutanua mtandao wa mabomba kwa kilometa 127.8 maeneo ya Ndevelwa, Mwinyi, Kidatu, Cheyo, Malolo, Kakola na Ifucha)	42,109,224	354,281,578	518,804,443
Kubadili dira za wateja 2158 zilizoharibika	-	-	117,027,510
Kukarabati kitumi cha kupimia dira za maji na ununuzi wa vifaa mwambata (kwa ajili ya kupima umadhubuti wa dira za maji)	12,357,201		
Kukarabati chemba za majimaeneo yote ya mji wa Tabora	18,000,220	110,581,945	229,259,113
Kununua Kompyuta 5 za mpakato na kompyuta 3 za mezani	-	-	24,308,000
Kununua vifaa vya umeme (taa za barabarani za umemejua kwa ajili ya Igombe, Kazima na Kazehill)	32,505,280		-
Ukarabati wa jengo moja la ofisi na majengo manne ya makazi Kazima na Kazehill	-	109,385,316	190,811,521
Kukarabati wa ghala kuu na ofisi kuu ya zamani	-	50,786,040	102,290,712
Kukarabati wa njia ya majitaka urefu wa kilometa 1 kutoka Kazehill kwa ajili ya usafi wa mazingira	-	58,599,276	118,027,745
Jumla ndogo	154,971,925	1,124,625,964	2,235,658,683
Uwekezaji Mpya			
Kununua 836.8 valves ranges 50mm-300mm kwa ajili ya utanzu wa mtandao	14,880,047	79,732,096	160,592,417
Kununua kifaa cha kupunguza maumzi ya umeme Igombe, Kununua, VSDs mbili zenye uwezo wa 160kW motor kila moja, na VSD moja yenye uwezo wa 315kW motor	-	-	217,540,625
Kununua kifaa cha kisasa cha mawasiliano chenye uwezo wa kurekodi malalamiko ya wateja na kununua vifaa vya matangazo	15,121,255	-	-

Amri ya Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Tabora (“Tabora Wssa”), ya Kurekebisha Bei ya Huduma za Majisafi na Usafi wa Mazingira
Tangazo La Serikali Na. 154 (Linaendelea)

Kununua na kufunga dira 1468 za malipo ya kabla kwa ajili ya kuongeza ufanisi katika ukusanyaji wa mapato	-	88,138,480	343,121,359
Kununua a kufunga dira kuu za maji (<i>bulk meters</i>) 41 za DN80mm -DN300mm na kujenga vizimba 60	32,060,366	11,040,104	22,236,427
Kutanua mabomba ya majitaka kwa urefu wa kilometa 3 sehemu za Gongoni, Kiloleni na Boma.	-	-	31,408,879
Kununua ardhi kwa ajili ya kujenga mabwawa ya kutuamisha majitaka sehemu za Masimba na Tumbi (kila moja likiwa na eneo la ekari 35)	-	99,034,290	
Kununua vifaa vya karakana ambavyo ni mashine mbili za kuunga vyuma, <i>Air Compressor</i> moja na mashine ya kuondolea maji (<i>Dewatering pump</i>)	-	-	109,386,000
Kujenga nyumba 3 za makazi Igombe	-	144,118,704	310,422,580
Kununua ghari moja la kubeba majitaka (5m3)	-	185,427,732	-
Kununua na kufunga kamera za CCTV, Skana, <i>Mobile stations</i> , na vifaa vya <i>GIS</i> kwa ajili ya ofisi, maghala, maeneo ya uzalishaji na vituo vya usamabazaji	25,314,754	11,568,040	
Usanifu wa mtandao wa majitaka na kujenga kifereji/kizimba cha kutolea masalia	4,666,079	25,002,358	50,358,504
Kujenga kilometa 13 za mtandao wa majitaka maeneo ya Kiloleni, Cheyo na Mabatini	18,107,301	97,024,762	86,036,444
Jumla ndogo	110,149,802	741,086,565	1,331,103,235
Jumla Kuu	265,121,727	1,865,712,529	3,566,761,918

*Amri ya Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Tabora (“Tabora Wssa”), ya Kurekebisha Bei ya Huduma za Majisafi na Usafi wa Mazingira
Tangazo La Serikali Na. 154 (Linaendelea)*

JEDWALI LA TATU

(Limetengenezwa chini ya aya ya 3(d))

VIASHIRIA VYA UTENDAJI (2020/21 – 2022/23)

Maelezo	Uniti	Lengo la Utendaji		
		2020/21	2021/22	2022/23
Idadi ya wateja wapya wa maji safi	Na	1,620	2,850	1,820
Kiwango cha upotevu wa maji	%	26	25	24
Wateja wenye Dira	%	100	100	100
Kiwango cha ufanisi katika ukusanyaji wa mapato	%	95	96	96
Wastani wa Saa za Utoaji wa Huduma ya Maji	Na. kwa Siku	22	23	24

JEDWALI LA NNE

(Limetengenezwa chini ya aya ya 3(g))

MAHITAJI YA FEDHA YALIYOINDHINSHWA

MAELEZO	SHILINGI MILIONI		
Gharama za Uzalishaji wa Maji	5,005.85	5,222.95	5,484.85
Gharama za Usambazaji wa Maji	810.31	1,062.24	1,159.37
Gharama za Huduma za Majitaka	74.58	73.80	92.41
Matengenezo ya muindombinu	869.83	1,369.98	2,068.78
Gharama za Wafanyakazi	2,517.94	2,583.95	2,651.44
Utawala	1,114.50	1,080.97	1,132.48
Matangazo	39.98	41.98	44.08
Matukio	44.72	46.96	49.30
Jumla ya Gharama za Uendeshaji na Matengenezo	10,477.71	11,482.82	12,682.71
Gharama za Uwekezaji	265.12	1,865.71	3,566.76
Jumla ya Gharama Zote	10,742.83	13,348.54	16,249.47
Mapato Yasiyotokana na Mauzo ya Maji	1,604.73	1,723.97	1,841.27
MAHITAJI YA MAPATO KUTOKANA NA MAUZO YA MAJI	9,138.10	11,624.56	14,408.20

Dodoma,
....., 2022

GODFREY H. CHIBULUNJE
Mkurugenzi Mkuu